

Haki ya mafunzo ya kinorwej na elimu jamii bila malipo

Kibali chako cha kuishi hapa Norway kinakupa haki ya mafunzo ya kinorwej na elimu jamii bila malipo.

Wasiliana haraka iwezekanavyo na idara ya mafunzo ya watu wazima katika manispaa pale ulipoandikishwa kuwa ndipo unapoishi ili uweze kijiungu na mafunzo, au kama unataka kutuma maombi ya kuruhusiwa usijiunge na masomo

Tarehe za mwisho za kupewa mafunzo bila malipo zinakadiria kuanzia wakati ulipopewa kibali cha kuishi hapa, au tangu ulipoingia Norway ukiwa na kibali cha kuishi hapa. Tarehe za mwisho ni miaka mitatu ikiwa hujafuzu elimu ya sekondari ya juu kabla hujaingia hapa, lakini pia ikiwa ulishafuzu sekondari ya juu, basi tarehe za mwisho ni miezi 18.

Wajibu wa mafunzo ya kinorwej na elimu jamii

Unawajibika kufuzu mafunzo ya kinorwej na elimu jamii ili uweze kupata kibali cha kudumu cha kuishi hapa, na/au kupata uraia. Waweza kuomba ruhusa ya kutowajibika kufanya mafunzo ikiwa waweza kuonesha ushahidi wa uwezo wako wa lugha ya kinorwej au kisami na elimu jamii, vinginevyo waweza kuthibitisha sababu maalumu za afya au sababu nyingine zenye uzito zinazokufanya ushindwe kufanya wajibu huu.

Haki na Wajibu wa mafunzo ya lugha ya kinorwej na elimu jamii

Haki na wajibu wa mafunzo unakuhusu hadi pale utakapofikia kiwango cha chini cha lugha ya kinorwej. Kiwango hiki kinawekwa na manispaa. Mafunzo haya hutolewa bila malipo hadi ufikie kiwango cha chini. Ikiwa unapewa ruhusa ya kutohudhuria mafunzo, basi tarehe zako za kuwa mafunzoni zinasogezwa mbele.

Maelezo muhimu

Ikiwa una swalii au unahitaji maelezo yanayohusiana na tarehe za mwisho na haki zako, wasiliana na mafunzo ya watu wazima. Waweza pia kupata maelezo hapa www.imdi.no na www.udi.no